KIPOK GIRLS SECONDARY SCHOOL
S.L.P 151
**MONDULI.**
08/12/2023

**Kumb Na.MOND/KIPOK/SS/12/01**

Jina la mwanafunzi...........................................................................................................................

**YAH:** MAAGIZO YA KUJIUNGA KIDATO CHA KWANZA 2024 SHULE YA SEKONDARI YA WASICHANA **KIPOK** WILAYA **MONDULI** MKOA WA **ARUSHA**.

1. **Utangulizi**

Ninafurahi kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga kidato cha kwanza katika shule hii mwaka 2024. **Shule ya Sekondari Kipok** ipo kata ya MOITA umbali wa kilomita 09 Kusini-Mashariki mwa kituo cha mafuta **waya** (PANONE) Kilichopo kati ya Kisongo na Duka Bovu.

Unatakiwa kuripoti shuleni tarehe 08**/01/2024**, kuanzia saa 2:00 kamili(saa mbili) asubuhi hadi saa 9:30 (saa tisa na nusu) alasiri, tayari kwa kuanza masomo.

2. **Mambo muhimu ya kuzingatia**

I. Sare za shule

a. Sare ya shule ni **sketi** mbili(2) ndefu sentimita ishirini(20) kutoka kwenye goti kushuka chini, rangi ya "kijani ya jeshi **" (01**) yenye **marinda** ya kawaida, **Suruali** rangi ya kijani ya jeshi (01)" inayofanana na Sketi kwa ajili ya kuingilia darasani (**Rangi ya kitambaa imeambatanishwa),mashati** mawili(2) meupe ya mikono mifupi,soksi ndefu nyeupe pea mbili,viatu vyeusi vya kufunga kamba , sweta rangi ya kijani ya jeshi lenye **V** mbele,**uzi umeambatishwa.**

b. **Tai** rangi ya kijani ya jeshi yenye miraba meupe (sample ya kitambaa imeambatanishwa)

c. **Gauni la solo la rangi ya kijani ya jeshi,kitambaa kimefanana na sketi ya shule.**Kitambaa kimeambatanishwa.(urefu sentimita ishirini chini ya goti).Gauni hili ni kwa ajili ya kushindia (shamba dress).Pia aje na pull neck nyeusi

d. Kwa wanao vaa Hijab/Waiisilamu, Rangi ya Hijab ifanane na sare za shule. **Nyeupe** kwa ajili ya darasani na **kijani ya jeshi** kwa ajili ya kazi za nje, inayoishia kwenye mabega.

e. Track suit rangi ya **kijani ya jeshi** yenye mistari meupe pembeni na raba rangi yoyote.

II. Daftari "Counter book"**kumi na mbili (12)** kalamu na mkebe wa majaribio wa hesabu**(Mathematical Set), Rimu moja yenye karatasi nyeupe** zake binafsi kwaajili ya kufanyia majaribio ya kila mwezi.

III. Wazazi wawapatie wanafunzi nauli ya kwenda shuleni na kurudi nyumbani wakati wa likizo, godoro nchi $2\frac{1}{2}$ **kwa 6** shuka mbili(2) rangi ya pinki,mto, chandarua cha kujikinga na mbu pamoja na blanketi.

IV. Mahitaji mengine sahani, kikombe,bakuli, kijiko, ndoo mbili(2) kwa ajili ya kufulia na kuogea,**buti** kwa ajili ya kipindi cha mvua,sanduku la chuma kwa ajili ya kutunzia vifaa vyake, pamoja na mahitaji mengine muhimu binafsi.

**Tunawashauri wazazi muwawekee watoto alama kwenye nguo na vifaa vingine, ili kuepuka kubadilishana.**

V. Kila mzazi ampatie mwanae fedha za matumizi, na ifahamike kwamba jukumu lamatibabu kwa mwanafunzi awapo shuleni ni la mzazi, shule inatoa huduma ya kwanza tu. Hivyo tunawashauri wazazi wawakatie wanafunzi **BIMA** ya afya ya **NHIF** na **CHF** ili iweze kumsaidia akiwa shuleni kwa ajili ya matibabu.

VI. Aje na kamusi ya kingereza"OXFORD"(**English to English dictionary**) kwa ajili ya matumizi yake binafsi.Aje na ufagio wa Chelewa mmoja kwa ajili ya kufanyia usafi wa mazingira kwenye eneo lake atakalopewa.

**"Wanafunzi hawaruhusiwi kabisa kutumia simu wawapo shuleni".**
**Endapo mzazi atalazimika kufanya mawasiliano kuhusu mwanae, tumia namba zifuatazo tuu na siyo vinginevyo.**

**0762-093-347 / 0683-557-760 Edward Thomas Laizer (Mwalimu wa taaluma)**

**0658108835 Caroline S. Mollel (Matron)**

**0684-042-118 Emelitha Negelo ( Mwalimu wa Chakula)**

**0684-682-536 0712 -693-003 Mohamed Mhaka Chambega (Makamu Mkuu Wa Shule)**

**0688-588-588 Daudi M Bonaventura ( Mwalimu wa nidhamu)**
**0693-177- 680 Amina Hassan (Matron )**

**Wanafunzi hawatakiwi kuja na nguo za nyumbani kabisa ila wanaruhusiwa kuja na kanga moja, kitenge kimoja au Taulo kwa ajili ya kuogea tu na sweta jeusi lisilo na maandishi kwa ajili ya baridi usiku wakati wa kujisomea usiku**

**NB:**

1. **Mwanafunzi asiyeripoti shuleni hadi ifikapo tarehe 23/01/2024 mzazi/mlezi atakamatwa na kuchukuliwa hatua kali za kisheria kwa kumnyima mtoto haki yake ya msingi ya kupata elimu.**

   **Aidha iwapo utampeleka mwanao shule ya binafsi(private) toa taarifa mapema kwa mkuu wa shule au katika ofisi ya Afisa Elimu Sekondari ili kuepuka usumbufu wa kukamatwa.**

2. **"Hairuhusiwi kabisa mwanafunzi kuja na vyakula shuleni"**

**3 Kikao cha wazazi kwa mwaka mara mbili**

**KARIBUNI SANA**

................................

**MKUU WA SHULE**
**0652278880**

HEADMISTRESS
KIPOK G R_S SEC. SCHO
P. O. Box 151 MONDU

3. **Sheria na kanuni muhimu za shule hii**

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu na Mafunzo wa Ufundi, yenye dhamana ya elimu nchini na Ofisi Rais-TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji Elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni.

a. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima;
b. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima;
c. Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni(preparation)
d. Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa;
e. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani ya na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
f. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule.
g. kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa.
h. kuzingatia ratiba ya shule wakati wote na
i. kutunza mali za umma

4. **Makosa yafuatayo yanaweza kusababisha kufukuzwa au kusimamishwa shule:**

a) wizi.
b) uasherati na ushoga.
c) ubakaji.
d) ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi, kuberi na kadhalika.
e) Kupigana au kupiga.
f) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.
g) Kudharau Bendera na Wimbo wa Taifa.
h) Kuwa mjamzito/kupata mimba.
i) Kuoa au kuolewa.
j) Kutoa mimba.
k) Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.
l) Kukataa adhabu kwa maksudi.
m) Kuwa na simu ya mkononi.

**5. Mambo mengine muhimu yanayopaswa kukamilishwa na kuwasilishwa shuleni na mwanafunzi:**

**A. FOMU YA UPIMAJI WA AFYA**

Medical Examination Form ambayo ijazwe na Mganga Mkuu wa hospitali ya Serikali. Fomu hii itakabidhiwa kwa Mkuu wa Shule mara utakaporipoti shuleni.(fomu imeambatanishwa)

**B. TAARIFA BINAFSI YA MWANAFUNZI**

Sehemu hii inahusu maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai.

Mimi.........................................................................ninakiri kwamba sitajihusisha wala kushiriki katika mgomo,fujo,makosa ya jinai wakati wote nikiwa mwanafunzi wa shule hii, Nitatii na kufuata sheria zote za shule ipasavyo.

Jina la mwanafunzi ...................................................................sahihi..................Tarehe...............

**C. TAARIFA ZA MZAZI/MLEZI**

Sehemuhii ni ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.

Mimi...............................................................ambaye ni mzazi/mlezi wa..........................................

Ninakiri na kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule wakati wote mtoto wangu akiwa katika shule hii.

Jina la mzazi...................................................................sahihi.........................tarehe.......................

❖ ***Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.***

**HALMASHAURI YA WILAYA YA MONDULI**
**SHULE YA SEKONDARI KIPOK GIRLS**
**TAARIFA YA MWANAFUNZI – KIDATO CHA .................. MWAKA ..................**

1. ShuleyaMsingialiyotoka: ………………………………………………………………………..
2. Jina la mwanafunzi: ……………………………………………… Jinsia: Me ……. Ke ……
3. TareheyaKuzaliwa: ……………………………………………….
4. Kijijiatokacho: ………………………………………………………….
5. Kata atokayo: …………………………………………………………….
6. Jina la mwenyekitiwakijiji au SerikaliyaMtaaatokako: ………………………………………………

   NambayaSimuyamwenyekiti ……………………………………………………..
7. Jina la Baloziatokako: ………………………………………………………………………

   NambayaSimu: …………………………………………………………………………
8. Jina la Baba/Mlezi: …………………………………………………………………….

   NambayaSimu: ……………………………………………………….
9. Jina la Mama/Mlezi: ……………………………………………………………………

   NambayaSimu: ………………………………………………………..
10. Jina la nduguwakaribu:

    (i) Jina la ndugu: 1 ……………………………………………………………..

    NambayaSimu: ………………………………………………

    (ii) Jina la ndugu 2: ………………………………………………………………

    NambayaSimu: ……………………………………………….

    (iii) Jina la ndugu 3: ………………………………………………………………

    NambayaSimu: ……………………………………………….

**Ninathibitishakuwataarifanilizojazahapojuunisahihi.**

**Jina: ............................................... Saini: ..................... Tarehe: ..................**

KIPOK GIRLS SECONDARY SCHOOL
P.O. BOX 151,
**MONDULI.**
DATE……………………………

**TO MEDICAL OFFICER,**
……………………………………
……………………………………
……………………………………

**PART A**
To be completed by Medical Officer in Government Hospital for all new entrants to secondary school.

Full Name: ……………………………………………………………………………………………………
Age: ……………………………………… Sex: …………………………………………………………

1. Hemoglobin ……………………………………………………………………………………
2. P.V. Bleeding …………………………………………………………………………………
3. Sight ……………………………………………………………………………………………
4. Blood pressure ………………………………………………………………………………
5. Urine for sugar ………………………………………………………………………………
6. Stool ……………………………………………………………………………………………
7. Asthma …………………………………………………………………………………………
8. Skin diseases …………………………………………………………………………………
9. Leprosy …………………………………………………………………………………………
10. Any deformity ………………………………………………………………………………
11. Epilepsy ………………………………………………………………………………………
12. Pulmonary tuberculosis……………………… ………………………………………
13. Neurosis ………………………………………………………………………………………
14. General diseases ……………………………………………………………………………
15. Pregnancy test ………………………………………………………………………………
16. Additional information or any other physical, health hereditably of infectious diseases ……………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………

**PART B:**
**(To be completed by a Governments Medical Officers**
I have examined the above named pupil and consider that he/she is physically and mentally fit/unfit to join to school.

**………………………………**
**Signature (Dr)**